

## TAARIFA YA TAFTISHI

### MWITO WA MKUTANO WA KUPATA MAONI YA WADAU WOTE KUHUSU MAOMBI YA SONGAS KUHUSU UTARATIBU WA KUREKEBISHA BEI YA HUDUMA YA KUSAFISHA NA KUSAFIRISHA GESI ASILIA

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*Energy and Water Utilities Regulatory Authority*, "EWURA") imepokea kutoka Songas **Ombi Na. TR-G-08-025** kuhusu utaratibu wa kurekebisha bei ya kusafisha na kusafirisha gesi asilia (**Tariff Adjustment Mechanism**).

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA (Cap 414), EWURA imeanzisha mchakato wa taftishi ili kupata maoni ya wadau wa Songas kuhusu uhalali wa maombi hayo ya kurekebisha bei ya huduma mpya ya kusafisha na kusafirisha gesi asilia kwa wenye viwanda na wazalishaji wa umeme, Dar es Salaam kuanzia mwezi Septemba 2010.

EWURA inatoa rai kwa wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi (kuunga mkono au kupinga) maombi haya, kujisajili kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyooneshwa hapo chini kabla ya **Jumatano, tarehe 24 Desemba, 2008** saa 11:00 jioni. Ikumbukwe kuwa, wadau watakojijisajili tu ndio watakaopewa fursa ya kutoa mada kuhusu maoni yao kwenye mkutano wa taftishi; aidha, watapokea nyaraka zote zitakazowasilishwa na mwombaji kwa kulipia gharama ndogo (zisizozidi TShs 25,000/=) za kudurufu na kuwasilisha nakala husika kwao. Wale wote watakaoshindwa kujisajili, watapata fursa ya kutoa mawazo yao papo hapo kwenye mkutano huo mara baada ya EWURA kusikiliza wadau waliojijisajili.

Kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu shirikishi ikiwa ni kanuni kuu ya udhibiti, unaarifiwa rasmi kwamba, EWURA imeandaa mkutano wa taftishi kukusanya maoni ya wadau wote, likiwemo Baraza la Ushauri la Wawakilishi wa Watumiaji Huduma za Nishati na Maji (Consumer Consultative Council, CCC), Baraza la Ushauri la Serikali (Government Consultative Council, GCC), vyombo vya habari, na wananchi wote kwa ujumla, utakaofanyika kwenye ukumbi wa **Karimjee Hall, Dar es Salaam, siku ya Jumatatu, tarehe 29 Desemba, 2008** kuanzia saa tatu (**3:00**) asubuhi.

Ndani ya siku saba (7) baada ya mkutano wa taftishi wa tarehe 29 Desemba 2008, siku yoyote na wakati wa saa za kazi (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 02:00 asubuhi hadi 11:00 jioni), EWURA itapokea maoni ya maandishi kutoka kwa wadau kabla ya hitimisho la uchambuzi wa kina halijafikiwa siku ya **Jumane tarehe 6 Januari, 2008**. Tafadhali zingatia tarehe zilizotajwa.

Licha ya nakala ya **Maombi Na.TR-G-08-025**, inayopatikana bure kwenye tovuti ya EWURA ([www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)), nyaraka za siri zilizowasilishwa na Songas kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya EWURA hazitatolewa. Nyaraka zilizobaki zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi katika ofisi za EWURA, na nakala za nyaraka za ziada zitapatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu kwenye anuani ifuatayo na kulipia gharama husika:-

**Director General**  
**Energy and Water Utilities Regulatory Authority**  
**6<sup>th</sup> Floor, Harbour View Towers,**  
**Samora Avenue**  
**P.O. Box 72175**  
**DAR ES SALAAM**

**Tel: +255 (0) 22 2123850/3/4/6, Fax: +255 (0)22 2123180, e-mail: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)**

---